




KUWA MWEREVU. TUMIA BARABARA NA WAENDESHA BAISKELI.

Madereva: Watu ambao wanaendesha baiskeli ni vigumu kuwatambua barabarani na wana ulinzi mdogo unaosababisha ajali ya trafiki. Tazama kioo cha nyuma kabla ya kusimama. Angalia sehemu za gari zisizoonekana kabla ya kugeuka, maegesho sambamba, kufungua mlango au kuondoa gari kando. Nyongeza juu ya kutumia kioo, tazama kwa kugeuza kichwa chako kuangalia waendesha baiskeli, skaters na waendesha pikipiki ambao wanaweza kuwa kando au kukaribia.

Vidokezo vya kushirikiana barabara na baiskeli

- **Endesha kwa uangalifu.** Punguza mwenda unapokaribia muendesha baiskeli. Usimfuate kwa ukaribu. Acha nafasi kati ya gari lako na baiskeli. Tambua hatari za waendesha baiskeli wanazoweza kukutana nazo na uwape nafasi.
- **Ruhusu Baiskeli.** Baiskeli zinazingatiwa kuwa magari na huendeshwa uelekeo sawa na magari. Toa kwa usahhi haki ya njia. Toa muda wa ziada kwa waendesha baiskeli kuvuka makutano ya barabara.
- **Kuwa na Busara.** Angalia baiskeli katika trafiki na makutano ya barabara. Usipige honi karibu na waendesha baiskeli. Angalia waendesha baiskeli unaposimama na kufungua mlango.
- **Pita kwa Uangalifu.** Wakati wa kupita, acha hatua nne kati yako na muendesha baiskeli. Subiri usalama wa barabara na hali za trafiki kabla hujaipita baiskeli. Angalia juu ya bega lako kabla ya kurudi nyuma.
- **Tazama watoto.** Watoto katika baiskeli mara nyingi hawatabiriki. Tegemea visivyotegemewa na kupunguza mwendo. Usitegeme watoto kujua sheria za barabarani. Kwasababu ya ukubwa wao, watoto wanaweza kuwa wagumu kuwaona.

Vidokezo kwa watu wanaoendesha baiskeli



- **Sheria ambayo inatumika kwa waendesha pikipiki ni hiyohiyo inayotumika kwa baiskeli.** Tii vifaa vote vya udhibiti wa trafiki (alama na taa) na tumia saini za mkono kuonesha kusimama na kugeuka.
- **Endesha upande wa kulia wa barabara.** Siku zote endesha uelekeo mmoja na trafiki. Tumia barabara ya mbali ya kulia. Baiskeli na magari yanayoenda polepole hubaki upande wa kulia.
- **Breki. Kengele. Taa.** Baisikeli lazima ziwe na breki zinazofanya kazi, honi au kengele na taa za mbele.

- **Mara zote vaa Kofia sahihi inayokaa.** Haishauriwi kuvaa kofia au kilemba kichwani wakati umevaa helimenti kwa kuwa zinapunguza ufanisi wa usalama wa helimenti.
- **Endesha Kiutabiri.** Endesha katika mstari ulionyooka na usiyumbe barabarani au katikati ya maegesho ya magari. Angalia trafiki kabla ya kuingia barabarani au makutano. Tarajia hatari na rekebisha nafasi kwa usalama.
- **Kuwa wazi.** Vaa nguo zenye rangi za kung'aa tofauti. Tumia mwanga mweupe wa mbele kwenye hali ya mwanga hafifu. Tumia mkanda au nguo zinazoonesha. Fanya mawasliano ya macho na waendesha pikipiki ili wakuone.
- **Abiria mtoto.** Umri wa miaka 1-4 lazima waendeshwe kwenye kiti salama kilichounganishwa. Sio sheria kuendesha mtoto wa umri chini ya mwaka moja kwenye baiskeli.
- **Simamia watoto.** Walezi wanategemewa kuwa na watoto nje na kusaidia watoto kujifunza kuendesha baiskeli na kujua sheria za trafiki. Watoto wanaruhusiwa kuendesha pembeni mwa barabara wakati wakiwa makini na watembea kwa miguu.

